SHULE YA SEKONDARI NTUCHI,
S. L. P. 169,
NAMANYERE – NKASI.
TAREHE----------

JINA LA MWANAFUNZI _____
S. L. P 169,
NAMANYERE – NKASI.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NTUCHI WILAYA YA NKASI MKOA WA RUKWA MWAKA 2020.

1.0.UTANGULIZI

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Ntuchi iliyopo umbali wa km 27 kusini mwa mji wa Namanyere katika kata ya Isale. Muhula wa masomo utaanza tarehe _____ na siku ya kuripoti ni tarehe _____mwisho wa kuripoti ni tarehe _____.

1.1.SARE YA SHULE

A. WAVULANA

- Suruali kijani Na.1 na dark blue Na.1
- Shati jeupe, fupi mikono
- Viatu vyeusi vya kamba, kisigino kifupi , soksi nyeusi
- Sweta la blue .
- T-shirt ya damu ya mzee
- Nguo za michezo T-shirt za njano, bukta na raba.

B. WASICHANA

- Sketi kijani Na.1 na dark blue Na.1
- Shati jeupe, fupi mikono
- Viatu vyeusi vya kamba, kisigino kifupi, soksi nyeupe
- Sweta la blue.
- T-shirt ya damu ya mzee
- Nguo za michezo Truck suit, T-shirt ya njano na raba

1.2.VIFAA VINGINE KWA WASICHANA WANAOKAA HOSTEL

- Ndoo ya kuogea,
- Godoro shuka jeupe na vifaa vingine vya malazi

1.3.MICHANGO YA CHAKULA KWA WANAFUNZI WA HOSTEL.

- Mahindi debe 8 na sado 2 kwa mwaka.
- Maharage debe 2kwa mwaka.
- Mafuta lita 3 kwa mwaka.
- Sukari kilo 4 kwa mwaka .
- Fedha sh.50,000/=kwa mwaka kwa ajili ya :-

Kumlipa mpishi, kusagia, kununua vyombo vya kupikia, Kununulia chumvi, kuni, vitu vingine vya jikoni n.k.

1.4. VIFAA VYA DARASANI (TAALUMA)

Daftari kubwa kumi(10), daftari ndogo kumi(10) kwa ajili ya mazoezi, kalamu za bluu au nyeusi, kalamu ya risasi(Penseli) Dictionary kwa ajili ya kujifunza kiingereza, mkebe (Mathematical set)na rula.

1.5. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa naWizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo, ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini maandalizi ya jioni (preparation) shuleni.
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kiadilifu (sio mlegezo/ nguo fupi).
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za umma.
j) Ni mwiko kwa mwanafunzi kutishia usalama au maisha ya mwalimu au mwanafunzi mwenzako.

1.6. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimam ishwa shule mara moja:-

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine, milungi, kuberi n.k
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau bendera ya taifana wimbo wa taifa
h) Kuoa au kuolewa
i) Kuwa mjamzito, Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
j) Kutoa mimba
k) Kugoma,kuchochea na kuongoza vulugu, au kuvunja amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

KARIBU SANA SEKONDARI YA NTUCHI"

.....

MKUU WA SHULE.

ESTHER N. KASANGA

0754 – 457 – 868 AU 0744 – 359 -185

MKUU WA SHULE
NTUCHI SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 109.
NKASI

OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.
SHULE YA SEKONDARI NTUCHI
S LP, 169 NAMANYERE-NKASI

FOMU YA KUKIRI UTII

Mimi..... ambaye nimechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Ntuchi nipo/sipo tayari kutii sheria na kanuni zote za shule kama zilivyooneshwa.Sahihi ..... Tarehe.....
Mimi ..... mzazi/mlezi wa .....
Nipo/sipo tayari kumpa huduma/mahitaji yote aweze kuendelea na masomo yake, shule ya Sekondari Wampembe .

Sahihi ..... Tarehe.....

.....
MKUU WA SHULE.
ESTHER N. KASANGA
0754 – 457 – 868 AU 0744 – 359 -185

MKUU WA SHULE
NTUCHI SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 169.
NKASI

"USIJE BILA KUKAMILISHA FOMU HII"UJE NAYO SIKU YA KURIPOTI

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PO- RALGA
NTUCHI SECONDARY SCHOOL,
SLP 169,
NAMANYERE-NKASI

TO THE MEDICAL OFFICER,
.....HOSPITAL,
BOX.....
.....
Please examine the student.....
The following:-

a) Epilepsy.....
b) Vision .....
c) Hearing .....
d) Pregnancy .....
e) Any other problem that can lead him / her not to be able for schooling/any other health problem that will require him/her to stay close to hospital.

DOCTOR'S DECLARATION.

I have examined the above mentioned student. He /she is fit/not fit for schooling.

Signature ..... Title.....
Date .....

"USIJE BILA KUKAMILISHA FOMU HII" NENDA NAYO HOSPITALI IJAZWE NA DAKTARI NA LAZIMA UIRUDISHE SHULENI